**HOTUBA YA MHE. MBONI MOHAMED MHITA, MKUU WA MKOA WA SHINYANGA,**

**KATIKA UZINDUZI WA MPANGO WA KITAIFA WA USAMBAZAJI WA MBEGU BORA KWA WAKULIMA KWA MPANGO WA RUZUKU, ULIOANDALIWA NA MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO (COPRA),**

**MKOA WA SHINYANGA – TAREHE 23 OKTOBA, 2025**

- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***
- ***David Lyamongi, Kaimu, Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga;***
- ***Kamati ya Usalama Mkoa;***
- ***Mkurugenzi Mkuu wa COPRA;***
- ***Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba (TCB);***
- ***Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB);***
- ***Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC);***
- ***Makatibu Tawala Wasaidizi Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga;***
- ***Makatibu Tawala Wilaya;***
- ***Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;***
- ***Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali;***
- ***Wadau wa Sekta Binafsi;***
- ***Viongozi wa Vyama vya Ushirika;***
- ***Wanahabari;***
- ***Wawakilishi Wakulima na Wageni Waalikwa;***
- ***Mabibi na Mabwana;***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana hapa siku hii muhimu. Pia, kwa namna ya pekee ninawashukuru Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA) kunipa fursa ya kuwa mgeni rasmi katika tukio hili muhimu ambalo linatuleta pamoja wadau muhimu wa mpango huu wakiwemo wafanyabiashara wa mazao,

wakulima na watendaji wa Serikali ambao ni wasimamizi muhimu wa mpangu huu.

***Ndugu washiriki,***

Leo ni siku ya muhimu kwa sekta ya kilimo nchini. Tumekusanyika hapa Shinyanga kwa ajili ya uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Usambazaji wa Mbegu Bora kwa Wakulima kwa Mpango wa Ruzuku, unaoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA). Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa maono ya Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia bora za kilimo kwa gharama nafuu ili kuongeza uzalishaji, kipato na tija kwa mkulima.

***Ndugu washiriki,***

Mbegu bora ni msingi wa kilimo chenye tija na uhakika wa chakula. Bila mbegu bora, hatuwezi kuwa na mavuno ya kutosha na yenye ubora unaohitajika; na hivyo juhudi za kuinua kipato cha wakulima zitabaki kuwa ndoto. Kwa kutambua umuhimu wa suala hilo, Serikali imeweka mkazo mkubwa katika kuhakikisha wakulima wanapata mbegu bora kwa bei nafuu kupitia mpango huu wa ruzuku. Hata hivyo upatikanaji wa mbegu nchini ni mdogo ikilinganishwa na mahitaji. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2025/2026 mahitaji ya mbegu kitaifa yanakadiriwa kufikia tani 127,650 wakati upatikanaji wake ni tani 105,000 za mbegu za mazao mbalimbali. Aidha, wakati Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha utoshelevu wa mbegu nchini, mpango wa ununuzi na usambazaji wa mbegu bora utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wake pamoja na upatikanaji wa fedha.

***Ndugu washiriki,***

Nimeelezwa kwamba kwa msimu wa kilimo wa 2025/2026, kiasi cha tani 192 za mbegu bora za mazao ya ufuta (tani 126); mbaazi tani 16; choroko (tani 17); dengu (tani 30); na soya (tani 3) zenye thamani ya shilingi **Bilioni 1.82** zitanunuliwa na kusambazwa kwa wakulima waliouza mazao hayo kupitia mifumo rasmi ya masoko ya kidigitali. Kwa Mkoa wa Shinyanga COPRA imetoa jumla ya tani 3 za mbegu za choroko ambazo zitasambazwa katika Halmashauri za Kishapu (tani 1.3), Shinyanga DC (tani 1.2) na Shinyanga Manispaa (tani 0.5).

Wakulima watakao nufaika na mbegu hizo, wanatakiwa wawe wamesajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku na wawe na namba ya usajili. Kadhalika, nimeelezwa kwamba usambazaji wa mbegu hizo utafanyika kupitia mfumo wa kidigitali ambao utasambazwa katika Halmashauri, lengo ni kuhakikisha uwazi, ufanisi na usawa katika usambazaji wake. Wito wangu kwa wakulima ni kuhakikisha wanahuisha taarifa zao kwenye mfumo ruzuku.

***Ndugu washiriki,***

Ugawaji wa mbegu kwa mpango wa ruzuku pia ni mkakati wa Serikali wa kuhamasisha matumizi ya mifumo rasmi ya masoko. Mifumo hii inahakikisha uwazi, usawa na ufanisi katika biashara. Aidha, mifumo rasmi pia inawezesha serikali kupata takwimu sahihi za mauzo na hivyo, Serikali kuweka mipango ya usimamizi na uendelezaji wa mazao hayo. Nitoe rai kwa wakulima wengine na wafanyabiashara wa mazao ya choroko, dengu, mbaazi, soya na ufuta kuhakikisha wanauza mazao yao kupitia mifumo rasmi ya masoko kwa kuwa mifumo hiyo inalinda maslahi yao.

***Ndugu washiriki,***

Nimeelezwa kuwa, sambamba na usambazaji wa mbegu, COPRA itaongeza nguvu katika huduma za ugani kwa kutoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo kwa wakulima ili kuimarisha ubora kwenye mazao haya. Vilevile, COPRA itasambaza viuatilifu kwa mpango wa ruzuku ya asilimia 50. Utekelezaji wake utafanyika kwa awamu ambapo kwa mwaka huu itaanzia kwenye zao la ufuta na baadae katika mazao mengine kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivyo, nawahimiza wakulima kutumia ipasavyo huduma hizi na kufuata kanuni bora za kilimo ili kuongeza mavuno na ubora wa mazao yao.

***Ndugu washiriki,***

Serikali itaendelea kuwa bega kwa bega na wakulima, kuhakikisha wanapata elimu ya kilimo bora, masoko ya uhakika na mazingira rafiki ya uzalishaji. Tunawahimiza wakulima kushirikiana na maafisa ugani, vyama vya ushirika na wadau wote wa kilimo ili kuongeza maarifa na mbinu za kisasa za kilimo bora.

Natoa rai kwa wadau wote wakiwemo watendaji wa Serikali na vyama vya ushirika kusimamia utekelezaji wa mpango huu kwa ueledi na uwazi ili matokeo yake yaonekane kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

**Ndugu washiriki,**

Napenda kutoa rai kuwa, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa utabiri wa mvua za msimu wa 2025/2026 kuwa chini ya wastani hadi wastani kwa maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka. Mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida na Dodoma inatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, huku Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Lindi na kusini mwa Morogoro

zikitarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba kwa wakati, kupanda mazao yanayostahimili ukame kama vile choroko, dengu, mtama, uwele, viazi vitamu na muhogo pia, kutumia mbegu bora zinazokomaa mapema na kufuatilia taarifa za hali ya hewa mara kwa mara ili kulima mazao kwa kuzingatia utabiri uliyotolewa. Pia, watendaji wa Serikali na Wakulima wanatakiwa kuchukua tahadhari na hatua madhubuti ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na utabiri huo.

**Ndugu washiriki,**

Aidha, ninapenda kuchukua fursa hii, kuwaelekeza kuwa tarehe 29 Oktoba 2025 ni siku muhimu ya kutimiza wajibu wetu wa kidemokrasia, siku ya kupiga kura na kuwachagua viongozi watakaounda Serikali ya awamu inayofuata. Kupiga kura si tu haki ya kikatiba, bali ni mchango wa moja kwa moja katika kuamua mwelekeo wa taifa letu. Hivyo basi, nitoe rai kwa wananchi wote wenye sifa, kujitokeza kwa wingi, kwa amani na utulivu, kushiriki zoezi hili la msingi kwa mustakabali wa nchi yetu. **NDUGU WANANCHI TWENDENI TUKAPIGE KURA.**

**Nikihitimisha,**

Napenda kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika maandalizi na utekelezaji wa mpango huu. Baada ya kusema hayo, natangaza rasmi kuwa Mpango wa Kitaifa wa Usambazaji wa Mbegu Bora kwa Wakulima katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026 umezinduliwa rasmi.

**Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**